

AML
FINANCE LIMITED

TAARIFA YA ELIMU YA KIFEDHA KWA WATEJA

Kuelewa Masharti ya Mkopo Wako



**AML Tower, Mwenge, Lufungira
Dar Es Salaam**



+255 677 700 330




www.amlfinance.co.tz

Kuelewa Masharti ya Mkopo Wako

AML Finance Limited tunajali sio tu kutoa huduma za kifedha bali pia kuhakikisha wateja wetu wanaelewa vizuri jinsi ya kuzitumia. Kuelewa masharti ya mkopo wako kutakusaidia kusimamia fedha zako kwa ufanisi na kuepuka gharama zisizo za lazima. Ili kukusaidia kuelewa vizuri zaidi, yafuatayo ni maeneo muhimu ya kuzingatia katika masharti ya mkopo wako:






AML
FINANCE LIMITED

1. Muda wa Mkopo

Muda wa mkopo ni kipindi ulichokubaliana na mkopeshaji kumaliza kulipa mkopo wako wote. Hutegemea aina ya mkopo na makubaliano yaliyofanyika baina ya pande mbili.

Muda huu huathiri marejesho yako: **mkopo wa muda mfupi** huwa na malipo makubwa ya kila mwezi lakini riba ndogo kwa ujumla, wakati **mkopo wa muda mrefu** huwa na malipo madogo ya kila mwezi lakini riba huongezeka.





AML
FINANCE LIMITED

Ushauri wetu:

Chagua muda wa mkopo unaoendana na kipato chako ili uweze kulipa kwa wakati bila changamoto.

Mfano:

- Ukikopa TZS **10,000,000** kwa riba ya **4.5%** kwa mwezi unaweza kulipa takribani TZS **3,638,000/=** kwa mwezi kwa miezi **3**, au TZS **1,939,000/=** kwa mwezi kwa miezi **6**. Kama kipato chako kinamudu TZS **3,638,000/=**, mkopo wa muda mfupi utakusaidia kupunguza gharama ya riba.



2. Riba (Gharama ya Mkopo)

Riba ni gharama unayolipa kwa kutumia mkopo.

Unapochukua mkopo, haulipi tu kiasi ulichokopa; unalipa pia gharama ya huduma hiyo, ambayo ndiyo riba.

- Huhesabiwa kama asilimia ya kiasi cha mkopo
- Inaweza kutozwa kila mwezi kulingana na makubaliano ya mkopo





Ushauri wetu:

Hakikisha unaelewa vizuri namna riba inavyokokotolewa kabla ya kuchukua mkopo. Kulipa kwa wakati kutakusaidia kupunguza gharama ya mkopo.

Mfano:

Kama mkopo wako una riba ya **4.5%** kwa mwezi kwa TZS **10,000,000**:

- Utalipa TZS **450,000** kama riba kila mwezi
- Ukichelewa kulipa, gharama inaweza kuongezeka

Kulipa kwa wakati hukusaidia kudhibiti gharama hizi.



3. Riba ya ucheleweshaji wa malipo

Riba ya ucheleweshaji wa malipo ni gharama ya ziada anayotozwa mkopaji pale anaposhindwa kutimiza masharti ya mkopo kama yalivyokubaliwa. inaweza kujumuisha:

- Gharama za kuchelewa kulipa marejesho.
- Gharama za malipo pungufu ya kiasi kilichotakiwa kulipwa.
- Gharama nyingine kama zilivyoainishwa kwenye mkataba wako.

Adhabu zinaweza kuathiri uwezo wako wa kulipa kwa sababu zinakuongezea mzigo wa kifedha. Pia, kuchelewa mara kwa mara kunaweza kuathiri historia yako ya mikopo na kupunguza nafasi yako ya kupata mikopo mingine baadaye.



Ushauri wetu:

Hakikisha unalipa marejesho yako kwa wakati na kwa kiasi kilichokubaliwa. Kama unaona unaweza kuchelewa kulipa, ni vyema kuwasiliana na mkopeshaji mapema ili kupata ushauri au kupanga namna bora ya kulipa kabla adhabu haijaongezeka.

Mfano:

Kama malipo yako yanatakiwa kufanyika kila tarehe 5 ya mwezi na ukachelewa:

- Utatozwa gharama ya kuchelewa.
 - Kuendelea kuchelewa kunaweza kuongeza deni lako na kuathiri uwezo wako wa kupata mkopo mwingine
- Kuwasiliana mapema kunaweza kukusaidia kuepuka gharama hizi.







AML
FINANCE LIMITED

Mambo Muhimu ya Kuzingatia



- Kopa kulingana na uwezo wako wa kulipa
- Elewa masharti yote kabla ya kukubali mkopo
- Lipa kwa wakati ili kuepuka gharama za ziada
- Wasiliana na mkopeshaji wako mara kwa mara





AML
FINANCE LIMITED

Tuko Tayari Kukuhudumia:

Kwa maelezo zaidi au msaada,
tafadhali tembelea ofisi zetu au
wasiliana nasi.

Tupo tayari kukuhudumia wakati wote.

AML Finance Limited

Upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wote

